

Sheria Ndogo Za (Usafi wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoa

TANGAZO LA SERIKALI Na 510 la tarehe 14/9/2018

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)

(SURA YA 288)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya Kifungu cha 89

SHERIA NDOGO ZA (USAIFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA MJI KONDOA,
MWAKA 2018

SEHEMU YA KWANZA

UTANGULIZI

Jina na Tarehe
ya kuanza
kutumika

Matumizi

Tafsiri

- 1 Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Mji Kondoa za Mwaka 2018 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.
- 2 Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Mji Kondoa.
- 3 Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo; -

“Afisa Mwidhiniwa” maana yake ni Afisa yeoyote wa Umma atakayeteuliwa na Halmasaauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

Sheria Ndogo Za (Usafi wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea.)

“Afya” maana yake ni hali timilifu ya kimwili,
kiakili na kijamii

“Chakula” maana yake ni kitu chochote
kinacholiwa na kunywewa na binadamu
isipokuwa madawa, hii ni pamoja na:-

- (a) kitu chochote kinachotumika katika
matengenezo ya chakula;
- (b) kitu chochote kinachoongeza ladha ya
chakula;
- (c) kitu chochote kinachobadili rangi ya
chakula (binzari n.k);

“Choo cha kuvuta” maana yake ni choo ambacho
kimejengwa na kuunganishwa na maji na kuwa na
tanki ya kusukuma maji kwa ajili ya kuondoa
uchafu hadi mahali palipoandaliwa;

“Choo bora” maana yake ni choo chochote cha
maji chenye sakafu, banda imara la kudumu,
lililoezekwa, lenye mlango imara, bomba la
kutolea hewa chafu na lenye mfuniko kwenye
tundu la choo na shimo salama na safi kwa ajili ya
kutupa kinyesi na mkojo wa binadamu,
lililojengwa kwa vifaa vya kudumu, lenye vipimo
vya futi 4×3 na kimo cha futi 12 na zaidi;

“Choo cha Umma” maana yake ni choo
kilichoengwa na Halmashauri au wakala wake
kwa matumizi ya umma;

“Eneo la wazi” maana yake ni eneo lililo chini ya
Halmashauri ambalo limekatazwa kufanyia
shughuli ambayo haihusiani na matumizi
yaliyokusudiwa.

Sheria Ndogo Za (Usafi wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea.)

“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Mji Kondoa.

“Hati ya usafi” maana yake ni hati itakayotolewa na Afisa Muidhiniwa inayothibitisha kukaguliwa kwa maeneo yote yaliyotajwa katika Sheria Ndogo hizi kulingana na Kanuni za Afya.

“Jengo la biashara” maana yake ni jengo lolote lililojengwa na kuidhinishwa na Halmashauri kufanya biashara iliyokusudiwa.

“Kaya” maana yake ni familia ya watu akiwemo baba, mama, mtoto au watoto na mtu mwingine ye yote anayeishi na familia hiyo, au watu wanaokaa katika nyumba moja na kuishi kama familia au mtu ye yote anayeishi peke yake katika chumba au nyumba.

“Kero au chukizo” maana yake ni kitu chochote ambacho kipo katika hali yoyote iwe kinatumika, kimewekwa, kimejengwa, au ni kichafu kiasi cha kusababisha:-

- (a) hatari kwa viumbe na maisha ya binadamu.
- (b) harufu mbaya na kuudhi.
- (c) kuzaliana kwa wadudu na wanyama hatari kama vile nzi, mende, sisimizi, panya, nyoka, nyuki, kunguni au viumbe wengine hatari;
- (d) magonjwa kwa binadamu, kuhifadhi mbu, nzi, panya na viumbe wenye madhara;

Sheria Ndogo Za (Usafi wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea.)

“*Kituo cha taka*” maana yake ni kizimba cha taka kilichowekwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kuweka taka ngumu kabla ya kusafirishwa hadi kwenye dampo la taka ngumu la Halmashauri;

“*Maji taka*” kama ilivyo katika Sheria ya Mazingira 2004 ni pamoja na taka zinazotokana na kinyesi, mkojo na jasho, uchafu wa majimaji kutoka majumbani, taasisi, majengo ya biashara na viwandani;

“*Mazao au mimea mirefu*” maana yake ni mazao au mimea inayozidi sentimita 15 kwenda juu kama vile Mtama, Mihogo, Mahindi, Mbaazi, Uwele na mengine yote yale yanayofanana na hayo;

“*Mkazi*” maana yake ni mtu yejote anayeishi katika eneo la Halmashauri na ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri.

“*Mmiliki*” maana yake ni mtu yejote ambaye ana miliki ardhi, sehemu za starehe, nyumba za kulala wageni, nyumba za kuuzia vyakula, kumbi za starehe, mpangaji, wakala wa mpangishaji wa nyumba au jengo na makazi yoyote katika mtaa, endapo mazungira husika ni mtaa au barabara za mtaa;

“*Mkurugenzi*” maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa pamoja na Afisa yejote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

“*Mzalishaji wa taka ngumu*” maana yake ni mtu yejote, kaya, taasisi, biashara, kiwanda ambaye

Sheria Ndogo Za (Usafi wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea.)

katika kutekeleza shughuli zake huzalisha taka.

“*Pipa la taka*” maana yake ni chombo chochote chenye mfuniko kinachowenza kuhifadhi taka ngumu zinazozalishwa majumbani, sehemu za biashara, maofisini ili zisisambae na kuchafua mazingira.

“*Taka*” kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, 2004 maana yake ni kitu chochote kimiminika, kigumu, gesi na mionzi, kinachotoa harufu mbaya, au kilichohifadhiwa katika mazingira ya hali ya ujazo, uozo au hali nyingine yoyote inayosababisha uharibifu wa mazingira, ambayo inajumuisha taka.

“*Taka Ngumu*” kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa mazingira, 2004 ni taka ambazo haziko katika umajimaji kutoka majumbani, katika majengo ya biashara, viwandani na kutoka katika shughuli za kilimo, pamoja na taka za vyakula, karatasi, plastiki au taka laini zinazotokana na ujenzi au ubomoaji majengo utengenezaji bustani na shughuli za uchimbaji madini, mizoga ya wanyama na mabaki ya magari mabovu (scraps).

“*Taka za Majumbani*” maana yake itajumuisha mabaki ya chakula, maganda ya matunda, majivu, kinyesi cha mifugo, taka za bustani, marapurapu ya nguo, karatasi za aina mbalimbali na vitu vingine ambavyo baada ya kuvitumia hutupwa.

“*Taka za Viwandani*” kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, maana yake ni uchafu unaotokana na uzalishaji viwandani au uchafu usiotokana na uzalishaji viwandani ambao ni chanzo cha nishati,

Sheria Ndogo Za (Usafi wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea.)

maji, mimea iliyotiwa dawa, au mawasiliano, pamoja na taka nyinginezo ngumu kama zilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, 2004 sehemu ya IX.

“*Uchafu Hatari*” kama iliyotafsiriwa katika Sheria ya Mazingira Na 20 ya mwaka 2004, maana yake ni kitu chochote kigumu, chenye majimaji, gesi au taka zitokazo viwandani, au mafuta machafu, ambayo yanaleta athari za kikemia kwa binadamu au mazingira.

“*Uchunguzi wa Afya*” maana yake ni hali ya mtu kupima afya yake kwa kuchukuliwa vipimo vyatatu na nje ya mwili ili kubaini kuwepo kwa vijidudu vyatatu magonjwa vinavyoweza kuleta maambukizi.

“*Ufugaji wa ndani*” maana yake ni ufugaji wa mifugo ndani ya eneo lililoruhusiwa tu.

“*Wakala*” maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, kampuni, taasisi au shirika aliyyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

SEHEMU YA PILI

USAIFI WA MAZINGIRA

Wajibu wa
kufanya usafi
wa mazingira

4. Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi au mfanyabiashara anayemiliki eneo la nyumba kuhakikisha kwamba anafanya usafi wa mazingira yanayozunguka makazi au eneo lake kwa kuhakikisha kwamba; -
- (a) majani yanayozunguka nyumba yake yanakatwa au kupaliliwa katika eneo lote

Sheria Ndogo Za (Usafi wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea.)

hadhi mwanzo wa mipaka ya barabara ya
mbele ya nyumba yake au eneo lake;

(b) taka taka zitakusanywa, kuhifadhiwa na
kupelekwa katika eneo lililoruhusiwa na
Halmashauri;

Kushiriki
shughuli za
usafi wa
mazingira

5. (1) Kila siku ya Jumamosi ya kila wiki itakuwa ni siku ya Wananchi kushiriki katika shughuli za usafi wa mazingira katika maeneo ya Halmashauri.

(2) Ni wajibu wa kila Mwananchi kushiriki katika shughuli za usafi wa mazingira katika siku maalum zilizopangwa na Halmashauri na Mwananchi atakayekataa kushiriki katika shughuli za kufanya usafi atakuwa ametenda kosa.

(3) Kifungu cha (1) na cha (2) hapo juu hakiathiri wajibu wa kila Mmiliki wa nyumba au Kiwanja au eneo lolote kufanya usafi katika eneo hilo mara kwa mara.

Mimea mirefu
Mjini

6. Ni marufuku kwa mtu yeote kupanda au kuotesha mazao au mimea mirefu katika maeneo ya mjini pamoja na maeneo mengine yaliyozuiliwa na Halmashauri.

Usafi wa
mifereji ya maji
ya mvua

7. (1) Kila Mmiliki wa nyumba atatakiwa kuondoa uchafu kama vile mchanga, majani, nyasi au vitu vingine vinavyofanana na hivyo kwenye mfereji wa maji ya mvua unaozunguka au kupita kando ya nyumba yake au eneo la biashara yake, kiwanja chake na kuhakikisha mfereji huo unakuwa safi, na imara siku zote.

Sheria Ndogo Za (Usafi wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea.)

- (2) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeote kuweka biashara ya aina yoyote aidha kwa kuuza au kwa maonyesho katika mfereji au katika kibaraza cha nyumba.
- Uwekaji taa za nje ya nyumba 8. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba, mpangajji au mfanyabiashara kuweka taa yenye mwanga nje ya jengo analoishi au analolitumia kwa shughuli yoyote na atatakiwa kuiwasha wakati wa usiku.
- Wajibu wa kuondoa na kudhibiti mazalia ya mbu 9. Itakuwa ni wajibu wa mmiliki wa nyumba kuhakikisha kuwa hakuna mkusanyiko wa maji, maji machafu, takataka au kitu chochote cha majimaji au kigumu ambacho kinaweza kuruhusu kuwepo kwa mazalia ya mbu au wadudu wengine wenye madhara kwa afya ya binadamu.
- Biashara ya matunda na mbogamboga 10. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mfanyabiashara ya matunda au Mbogamboga kuhakikisha kuwa ana chombo maalum cha kuhifadhia maganda au mabaki ya bidhaa zake.
(2) Ni marufuku mtu yeote kufanya biashara ya matunda au miwa pemberi mwa barabara au katika maeneo yasiyoruhusiwa.
- Upulizaji dawa za kuua wadudu 11. (1) Mtu yeote atakayetaka kupulizia dawa za kuuwa Wadudu au wanyama waharibifu katika nyumba yoyote au mahali popote atalazimika kuomba kibali cha kufanya shughuli hiyo kutoka Halmashauri.
(2) Halmashauri itajiridhisha kwanza kwamba tahadhali zote zinazoweza kuathiri uhai wa viumbe hai wengine zimechukuliwa, na pia mtu

Sheria Ndogo Za (Usafi wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea.)

huyo anao utaalamu wa kupulizia dawa za kuuwa wadudu au Wanyama waharibifu.

Matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo

12. Matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo yataktakiwa kufanyika kwenye karakana, gereji au maeneo yaliyoruhusiwa baada ya kupata kibali rasmi kutoka Halmashauri.

Kuegesha magari mabovu

13. Ni marufuku kwa mtu yejote kuegesha gari bovu au kufanya matengenezo kwenye eneo la barabara, hifadhi ya barabara, njia ya waenda kwa miguu, mtaa, eneo la wazi au eneo lolote ambalo halikutengwa kwa shughuli hiyo.

SEHEMU YA TATU

UIMARISHAJI WA AFYA

Usalama wa maji ya kunywa

14. Ni wajibu wa kila mkazi wa eneo la Halmashauri kuhakikisha kwamba anakunyuwa maji safi na salama na yaliyochemshwa bila kujali yametoka kwenye chanzo gani cha maji.

Utengenezaji, na uuzaji vyakula

15. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yejote kutengeneza, kuchoma, kupika, kuchemsha au kufanya biashara ya chakula katika eneo lolote la Halmashauri mpaka awe ametimiza Masharti na Kanuni za afya na amepata kibali kutoka kwa Bwana Afya wa Halmashauri.

Uuzaji wa vyakula

16. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayeendesha biashara ya vyakula vya kupikwa au kukaangwa kuhakikisha kwamba vyakula hivyo vinahifadhiwa kwenye kabati dogo la kuhifadhi chakula

Sheria Ndogo Za (Usafî wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoa

Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea.)

lililotengenezwa kwa mbao safi na kuwekwa kioo
kuzuia nzi, vumbi na wadudu waletao madhara
kwa afya kwa binadamu.

- (2) Itakuwa ni marufuku kwa mtu ye yeyote kuuza
vyakula visivyopikwa vikiwa vimewekwa chini,
vyakula vyote vitatakiwa kuwekwa juu ya meza.

Amri ya zui o la
kufanya shughuli
mbalimbali wakati
wa Magonjwa ya
mlipuko

17. (1) Afisa Muidhiniwa anaweza kutoa amri ya kuzuia
shughuli yoyote isifanyike kama vile utengenezaji
wa vyakula, pombe, mijumuiko, sherehe na
mikusanyiko yoyote kwa kutangaza kwa njia ya
kipaza sauti, maandishi, au kuititia vyombo vy
habari endapo atakuwa na sababu ya kuamini
kwamba shughuli hiyo inaweza kusababisha
kuenea kwa magonjwa ya mlipuko na kuleta athari
kwa maisha ya binadamu au viumbe vingine hai
na mtu ye yeyote atakayekataa kutii amri iliyotolewa
atakuwa ametenda kosa.

- (2) Halmashauri haitahusika na hasara ye yeyote
itakayotokea kutokana na kukamatwa na
kuharibiwa kwa chakula, chombo au kifaa
chochoote kilichotumika baada ya kutolewa amri
ya kuzuia kufanya kwa shughuli hiyo.

Machinjio na
Maduka ya nyama

18. (1) Kila mamiliki wa Machinjio au duka la kuuzia
nyama atawajibika kuhakikisha kuwa; -

- (a) Mhudumu wa Machinjio au Duka la
nyama anavaa vazi maalum jeupe,
amepima afya na ameruhusiwa kwa kibali
na Halmashauri;
- (b) Anafanya shughuli hii kwenye jengo la
kudumu lililosakafiwa kwa marumaru
nyeue kwenye sakafu na kuta zote, lenye
chombo cha kutunza taka, lenye maji safi,
na vifaa safi vy aukatia nyama,

Sheria Ndogo Za (Usafi wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea.)

- (c) Ana mzani uliokaguliwa na kukubalika kutumika kupimia nyama.
- (2) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yejote kuchinja, au kuuza nyama ya aina yoyote katika maeneo yasiyokuwa machinjio au maduka ya nyama au katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri.
- Ufugaji Mjini 19. (1) Kila Mfugaji ataruhusiwa kufuga idadi ya mifugo ambayo atawea kuhudumia, isiyoleta kero kwa majirani, kwa kuzingatia Maelekezo yatakayotolewa na Halmashauri
- (2) Ni marufuku kwa mtu yejote kuacha mifugo au kusababisha mifugo kuzurura ovyo mitaani, kuchunga kwenye vyanzo vya maji, kwenye eneo la barabara, Hifadhi ya barabara, au kuchungwa kwenye eneo lolote lisiloruhusiwa.
- Usafi wa zizi 20. Itakuwa ni wajibu wa kila mfugaji kuhakikisha kwamba sehemu anayotumia kufugia-
- (a) inakuwa katika hali ya usafi wakati wote;
- (b) Anakusanya uchafu wowote utokanao na wanyama kama vile kinyesi, manyoya na nyasi au mabaki ya vyakula na kwenda kutupa kwenye dampo au kupelekwa shambani kama mbolea.
- Uendeshaji wa Hotel, Hostel na Shule 21. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba za kulala wageni, Mgahawa, Hoteli, Hosteli, Shule au nyumba za biashara kuhakisha anapata kibali cha afya kwamba amekidhi masharti ya afya kutoka Halmashauri kabla hajaanza kutoa huduma.
- (2) Wakati wowote Halmashauri ikijiridhisha kuwa Mmiliki hajakidhi masharti ya afya inaweza kuzuia kibali cha kutoa huduma ya Shule, Hoteli

Sheria Ndogo Za (Usafi wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea.)

au Hosteli mpaka hapo mmiliki atakapokuwa amekidhi masharti ya kiafya yaliyotolewa na Halmashauri.

Mahitaji ya nyumba ya wageni, Hotel na Hosteli

22. Kibali cha kuendesha biashara ya nyumba ya kulala wageni, mgahawa, Hoteli na Hosteli kitatolewa baada ya Halmashauri kujiridhisha kuwa mahitaji yafuatayo yamezingatiwa; -

- (a) mwanga na hewa ya kutosha;
- (b) nafasi na vifaa (samani) za kutosha;
- (c) uimara wa jengo;
- (d) kuna mfumo imara wa maji taka, na maji safi, na uhifadhi wa taka ngumu;
- (e) kuna vyoo na mabafu safi vya kutumika kwa jinsia zote;
- (f) kuna vifaa vya tahadhali na vya kuzima moto, na
- (g) ujenzi wa jengo umezingatia watu wenye mahitaji maalumu hasa wale mavu.

Upimaji wa afya

23. Kila Mhudumu wa hoteli, mgahawa, baa, bucha, machinjio, sehemu za kuokea mikate, nyumba za kulala wageni, grosari au mtu ye yeyote anayetengeneza chakula kwa ajili ya kuuza atawajibika kupima afya na kupewa kibali na Halamshauri.

Ada ya ukaguzi wa afya

24. Halmashauri itatoza ada ya ukaguzi wa afya kwa Mujibu wa viwango vilivyobainishwa na Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Mji Kondoa

Sheria Ndogo Za (Usafi wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea.)

SEHEMU YA NNE
UTUPAJI TAKA

- | | | |
|--|-----|---|
| Eneo la kutupa taka | 25. | Halmashauri itatenga eneo maalum kwa ajili ya kutupia taka na kutoa huduma ya uzoaji taka kwa malipo kutoka kwa wazalishaji wa taka hadi kwenye dampo. |
| Marufuku kutupa taka ovyo | 26. | Ni marufuku kwa mtu ye yeyote kutupa taka au uchafu wowote au kuacha takataka au uchafu kwenye nyumba, uchochoro, kiwanja, mfereji wa maji ya mvua, barabara au mahali popote pasipotengwa kwa shughuli hiyo. |
| Vikundi vya wazoa taka | 27. | Halmashauri itahamasisha uundaji wa Vikundi Jamii na kuvitambua ili kuviwezesha kufanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa mazingira katika mitaa baada ya kuingia mkataba na Halmashauri. |
| Kutupa taka katika sehemu maalum | 28. | Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi kuhakikisha kwamba anatupa uchafu, taka, maganda ya matunda, chupa za maji na mabaki ya vocha za simu katika vyombo maalum vilivyowekwa kwa ajili ya kutunzia taka katika maeneo maalum yaliyotengwa. |
| Magari ya abiria kuwa na vyombo vya kuhifadhi takataka | 29 | (1)Kila mmiliki wa Gari la abiria litakaloingia katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuwa na chombo cha kuhifadhi taka na kuhakikisha kwamba kila abiria anatupa taka kwenye chombo hicho.

(2)Itakuwa ni kosa kwa mmiliki au dereva au kondakta iwapo abiria aliyeo ndani ya gari atatupa kitu chochote barabarani au stendi.

(3)Endapo abiria atakamatwa akitupa takataka nje ya chombo cha usafiri, mmiliki au dereva au kondakta |

Sheria Ndogo Za (Usafî wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea.)

atawajibika kulipa faini ya papo kwa papo kama ilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi.

- | | | |
|--------------------------|-----|---|
| Uhifadhi maji taka | 30. | Kila Mmiliki wa nyumba, Kiwanda anatakiwa kuhakikisha kuwa analo karo la kuhifadhi maji taka na atawajibika kunyonya maji taka pale karo linapojaa. |
| Kutiririsha maji ya taka | 31. | Ni marufuku kutitirisha au kuelekeza maji, kutoka vyooni, bafuni, karoni, viwandani, kwenda barabarani, uchochoroni, mtoni, kwenye vyanzo vya maji, maeneo ya wazi, kwenye mfereji wa maji ya mvua au sehemu yoyote isiyotengwa kuhifadhi maji taka. |
| Uendeshaji wa Viwanda | 32. | Ni marufuku kuendesha shughuli za karakana, mashine ya kusaga nafaka, kuranda mbao, kukamua maji ya matunda, kuchomelea vyuma au kuendesha shughuli zozote za viwandani zinazozalisha maji machafu, vumbi, kelele au harufu mbaya, uchafu ambaao unaleta athari kwa binadamu na viumbe wengi katika maeneo ya makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za ujenzi. |
| Ada ya utozaji taka | 33. | (1)Halmashauri itatoza ada ya uzoaji taka kila mwezi kutoka kwa kila kaya, Wamilliki wa Nyumba za Biashara, Taasisi, na kampuni zilizopo ndani ya eneo la Halmashauri kwa viwango vilivyoainishwa katika jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2)Ada ya kila mwezi italipwa kila tarehe 30 ya kila mwezi ndani ya mwezi husika na italipwa kwa Afisa muidhiniwa ambaye atatoa stakabadhi ya malipo yatakayolipwa na atajaza katika rejista ya wazalishaji taka. |

Sheria Ndogo Za (Usafi wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea.)

- (3) Endapo Mzalishaji wa taka atashindwa kulipia gharama ya huduma ya uzoaji taka kwa kipindi cha miezi miwili mfululizo Halmashauri itamtaka kulipa deni hili na adhabu ya asilimia 50% ya ada anayostahili, akishindwa Halmashauri itamchukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani.
- Wafanyabiashara 34. (1) Kila mfanyabiashara katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri ya Mji atawajibika kulipa ada ya uzoaji wa takataka kama inavyooneshwa katika jedwali la kwanza A la Sheria Ndogo hizi.
(2) Makampuni, Viwanda na Taasisi zisizo za Serikali zitapaswa kulipa ada ya uzoaji taka kama ilivyoainishwa katika jedwali la kwanza B la Sheria Ndogo hizi.
(3) Kampuni yoyote mbayo haijaorodheshwa katika jedwali la kwanza B itawajibika kulipa ada hata kama haijaorodheshwa katika jedwali hilo.
- Uteuzi wa wakala 35. Halmashauri inaweza kuteua kampuni, kikundi, kikundi cha jamii au Mtu binafsi kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria Ndogo hizi.

SEHEMU YA TANO

UJENZI NA MATUMIZI YA VYOO

- Wajibu wa kua na choo na kukitumia 36. Itakuwa ni wajibu wa kila Mmiliki au Mpangaji wa nyumba ya makazi au Nyumba ya Biashara kuhakikisha kwamba nyumba yake ina choo safi, imara na madhubuti kwa matumizi ya wakazi wa nyumba hiyo na kuhakikisha kinatumika wakati wote.

Sheria Ndogo Za (Usafî wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea.)

- Umbali wa kujenga choo 37. Choo kinatakiwa kijengwe umbali wa mita sitini (60) kutoka kisima au chanzo chochote cha maji kinachotumika kwa matumizi ya Nyumbani.
- Vyoo nya umma 38. (1) Halmashauri inaweza kumruhusu mtu binafsi, vikundi nya watu au Taasisi kujenga vyoo nya Umma katika maeneo ambayo Halmashauri itaona kuwa kuna haja ya kufanya hivyo.
 (2) Vyoo hivyo vitamiliwi na Halmashauri au kwa ubia na wajenzi na vitakuwa ni nya kulipia kama itakavyokuwa imeelekezwa na Halmashauri katika mkataba wake na mawalaka watakaopewa kusimamia vyoo hivyo.
- Vyoo nya muda katika mikusanyiko 39. Itakuwa ni wajibu wa mtu, kikundi, Taasisi yenye lengo la kukutanisha watu, sherehe au sehemu yoyote ambayo itakutanisha watu kwa muda maalum endapo eneo hilo hakuna choo cha kudumu kujenga vyoo kwa matumizi ya wakati huo kwa idhini na usimamizi wa Halmashauri
- Uwezo wa kukagua 40. Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika jengo lolote wakati wowote wakati wa saa za kazi kukagua utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.
- Ilani ya kujenga choo 41. (1) Endapo katika ukaguzi wa afya itagundulika kuwa nyumba yoyote haina choo, choo kilichopo kimejaa au hakifai kwa matumizi ya binadamu, Afisa Muidhiniwa atatoa ilani ya siku thelathini kwa mmiliki wa nyumba au mpangaji akiainisha masharti ya kurekebisha hali hiyo.

Sheria Ndogo Za (Usafi wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea.)

- (2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha Sheria Ndogo hizi, Halmashauri inaweza kuamuru nyumba au jengo hilo lisitumike kwa shughuli za makazi au biashara hadi hapo hali hiyo itakapokuwa imerekebishwa.
- Ilani ya kuondoa kero
42. (1) Endapo Afisa Muidhiniwa atagundua kuwa eneo alilokagua lina kero yoyote atatoa ilani ya siku saba (7) kwa mmiliki wa nyumba, mpangaji, mtumiaji, na, au mtu ye yeyote anayehusika akimtaka kuondoa kero hiyo.
- (2) Mtu ye yeyote atakayeshindwa kutekeleza masharti ya ilani aliyopewa ndani ya muda ulioainishwa kwenye ilani atakuwa ametenda kosa.
- Uwezo wa kutoa adhabu ya papo kwa papo
43. Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kutoa adhabu ya papo kwa papo kwa mtu ye yeyote atakayekutwa amechafua mazingira kwa kukiuka taratibu zilizowekwa na Sheria ndogo hizi.
- Makosa
44. Itakua ni kosa kwa mtu ye yeyote ambaye; -
(a) Atamzuia au kujaribu kumzuia Afisa Mwidhiniwa asitekeleze wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hizi; au
(b) atamwaga takataka katika mtaa, mtaro wa maji ya mvua, uchochoroni, au mahali popote hadharani au katika eneo lolote la wazi bila idhini ya Halmashauri;
(c) ataendesha biashara ya pombe ndani ya nyumba ya makazi;
(d) atatiririsha maji machafu barabarani au katika eneo la nyumba ya jirani;

Sheria Ndogo Za (Usafi wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea.)

- (e) ataosha gari, kufua, kunywesha mifugo na kukoroga dawa za mimea ndani ya mito, mabwawa, lambo au ndani ya chanzo cha maji au kisima kinachotumiwa kwa matumizi ya binadamu;
- (f) atauza vyakula viliyopikwa bila kufuata taratibu za kiafya zilizowekwa na Sheria Ndogo hizi;
- (g) atafanya matengenezo ya gari, pipipiki na mitambo, kuendesha shughuli za viwanda katika maeneo ya wazi, makazi, barabarabi, uchochoroni, au katika maeneo yasiyotengwa kwa shughuli hizo bila kuzingatia taratibu za Mipango Miji;
- (h) ataenda haja ndogo au kubwa barabarani, uchochoroni, upenuni au mahali popote ambapo sio chooni;
- (i) atakwenda kinyume na Sheria Ndogo hizi.

SEHEMU YA SITA

UTHIBITI WA MIFUGO

Wajibu wa
Halmashauri

45.

Halmashauri itakuwa na wajibu wa:-

- (a) kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi wa ufugaji na kusimamia na kulinda mipaka ya ardhi ya kilimo na mifugo iliyobainishwa;
- (b) kuelekeza idadi ya mifugo ambayo kila mfugaji ataruhusiwa kuwa nayo;
- (c) kuanzishwa majosho ya mifugo kwa ushirikiano na wafugaji;

Sheria Ndogo Za (Usafi wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea.)

- (d) kuhamasisha wafugaji kuvuna mifugo yao mara kwa mara ili kubakisha idadi ya mifugo yenye kuleta tija;
- (e) kutoa elimu ya ufugaji wa kisasa ili kupata mifugo na mazao bora ya mifugo;

Wajibu wa
Mfugaji

46.

Itakuwa ni wajibu wa kila mfugaji kuhakikisha kwamba; -

- (a) Anapitisha mifugo yake kwenye njia maalum zilizotengwa kwa ajili ya mapitio ya mifugo wakati wa kwenda au kurudi malishoni, minadani au sehemu nginine yoyote.
- (b) Anaogesha na kuchanja mifugo yake kila mara na ili kuzuia magonjwa ya mifugo na magonjwa ya mlipuko.
- (c) Anaipatia mifugo yake malisho, maji ya kutosha na kuzingatia kanuni za usafirishaji, uuzaji na uchinjaji wa mifugo.
- (d) Anafuga mifugo kulingana na ukubwa wa eneo lake la malisho.
- (e) Atalazimika kutoa taarifa yoyote juu ya kutokea kwa magonjwa ya mifugo akiyaona au kuhisi au kuyatambua dhidi ya mifugo yake.
- (f) Atalazimika kuheshimu mipaka iliyotenganisha ardhi ya kilimo, mifugo, hifadhi za Taifa ,makazi,

Sheria Ndogo Za (Usafi wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoaa
Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea.)

maeneo ya Taasisi na maeneo mengine
ya wadau wa kilimo kama mazao ya
wakulima,

Taratibu za
kuogesha
mifugo

47. (1) Kila mfugaji atakuwa na wajibu wakuogesha mifugo yake kwenye majosho ya pamoja au ya binafsi kulingana na maelekezo ya Afisa mifugo wa Halmashauri.

- (2) Mifugo itaogeshwa mara mbili kwa mwezi, kila inapotoka mnadani, na kabla ya kuingia na kutoka nje ya Wilaya.

Usimamizi wa
Majosho

48. Halmashauri itaunda vikundi mbalimbali vitakavyosimamia uendeshaji wa majosho na taratibu za uogeshaji wa mifugo katika maeneo yao ndani ya Halmashauri.

Ushuru wa
kuogesha
Mifugo

49. Mifugo itakayoogeshwa katika majosho ya Halamshauri, itatozwa ushuru kwa mujibu wa viwango viliviyowekwa na Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Mji Kondoaa.

Kibali cha
kusafirisha
mifugo

50. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayetaka kusafirisha mifugo kutoka au kuingia eneo la Halmashauri kuwa na kibali maalumu kitakachoruhusu kufasirisha mifugo hiyo.
- (2) Kibali cha kusafirisha mifugo nje na ndani ya Halmashauri kitatolewa na Afisa mifugo wa Halmashauri, Kata au Kijiji baada ya kujiridhisha kuwa mifugo hiyo imeogeshwa na kupatiwa chanjo kabla ya kusafirishwa.

Mifugo
inayozurura

51. (1) Mifugo yoyote ile itakayokutwa inazurura bila ya kuwa na mchungaji, itakamatwa na

*Sheria Ndogo Za (Usafi wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoaa
Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea.)*

hovyo		kuhifadhiwa na Halmashauri na mwenye mifugo atatakiwa kulipa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) na shilingi elfu kumi (10,000/=) kwa kila mfugo, kwa kila siku itakayokuwa chini ya uangalizi wa Halmashauri pamoja na kwa kuachia mifugo yake kuzurura.
	(2)	Ni marufuku kwa mtu ye yeyote kuingiza mifugo kwenye shamba au kusababisha mifugo hiyo kuingia kwenye shamba lolote
Wajibu kwa Halmashauri wa kulipa fidia	52.	Halmashauri itakuwa na wajibu wa kulipa fidia ya hasara itakayosababishwa na Afisa Mwidhiniwa au Afisa ye yeyote kwa uzembe au makusudi wakati wa kukusanya Ada na Ushuru au wakati anatekeleza Sheria Ndogo za Halmashauri.
Makosa	53.	Mfugaji ye yeyote atakuwa ametenda kosa iwapo;- <ul style="list-style-type: none"> (a) atashindwa au kukataa kuogesha au kuchanja mifugo yake ili kuzuia magonjwa au; (b) atalisha mifugo yake kwenye maeneo ambayo hayakutengwa kwa ajili ya Malisho ya mifugo au; (c) ataruhusu mifugo yake kuzurura hovyo; (d) atazembea au kushindwa kutoa taarifa juu ya ugonjwa wa mifugo au; (e) atamzuia Afisa Mwidhiniwa au Afisa Ugani kutekeleza majukumu yake;
Kufifilisha kosa	54.	Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu ye yeyote faini isiyozidi shilingi laki tatu (Tsh.300,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi na

Sheria Ndogo Za (Usafî wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea.)

kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoambatanishwa kwenye jedwali la nne la Sheria Ndogo hizi na atatakiwa kulipa faini hiyo kwa mujibu wa Sheria

- Adhabu 55. Mtu yejote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elf hamsini (Tsh.50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili (12) jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

JEDWALI LA KWANZA

A: ADA ZA KUZOLEA TAKATAKA
(Limetungwa Chini ya Kifungu cha 33(1)

Na.	AINA YA BIASHARA	ADA KWA MWEZI	ADA KWA MWAKA
1.	Vilabu vya pombe za kienyeji	Tsh.1,000/=	Tsh.12,000/=
2.	Maduka ya rejarejaaa/jumla	Tsh.2,000/=	Tsh.24,000/=
3.	Mama, Baba lishe	Tsh.1,000/=	Tsh.12,000/=
4.	Ghala za mbao	Tsh.2,000/=	Tsh.24,000/=
5.	Restaurant/hotel	Tsh.2,000/=	Tsh.24,000/=
6.	Maduka ya jumla	Tsh.5,000/=	Tsh.60,000/=
7.	Nyumba za kulala wageni	Tsh.5,000/=	Tsh.60,000/=
8.	Mashine za kusaga na kukoboa nafaka	Tsh.4,000/=	Tsh.48,000/=
9.	Viwanda vya mikate	Tsh.3,000/=	Tsh.36,000/=
10.	Mashine za kuranda mbao	Tsh.4,000/=	Tsh.48,000/=
11.	Ofisi mbalimbali	Tsh.2,000/=	Tsh.24,000/=

Sheria Ndogo Za (Usafi wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea.)

Na.	AINA YA BIASHARA	ADA KWA MWEZI	ADA KWA MWAKA
12.	Bar/grocery	Tsh.5000/=	Tsh.60,000/=
13.	Viwanda vya uselemara	Tsh.2,000/=	Tsh.24,000/=
14.	Saloon/vinyozi	Tsh.2,000/=	Tsh.24,000/=
15.	Gereji	Tsh.5,000/=	Tsh.60,000/=
16.	Kuchoma mahindi	Tsh.500/=	Tsh.6,000/=
17.	Kuuza barafu	Tsh.500/=	Tsh.6,000/=
18.	Maduka ya nyama	Tsh.3,000/=	Tsh.36,000/=
19.	Madukaya kuchomelea/workshop welding	Tsh.5,000/=	Tsh.60,000/=
20.	Biashara zote ndogondogo	Tsh.500/=	Tsh.6,000/=
21.	Wauzaji mkaa jumla	Tsh.3,000/=	Tsh.36,000/=
22.	Vituo vya kujazia mafuta/Filling station	Tsh.10,000/=	120,000/=
23.	Zahanati binafsi	Tsh.5,000/=	Tsh.60,000/=
24.	Hospital/vituo vya Afya binafsi	Tsh.10,000/=	Tsh.120,000/=
25.	Ghala	Tsh.10,000/=	Tsh.120,000/=
26.	Viwanda vya kukamua mafuta	Tsh.10,000/=	Tsh.120,000/=
27.	Shule/Vyuo binafsi	Tsh.5,000/=	Tsh.60,000/=
28.	Mafundi cherehani	Tsh.1,000/=	Tsh.12,000/=
30.	Vizimba sokoni(kila kimoja)	Tsh.100/=	Tsh.1,200/=

B: MAKAMPUNI

Na.	JINA LA KAMPUNI/TAASISI	ADA KWA MWEZI	ADA KWA MWAKA
1.	NMB	Tsh.30,000/=	Tsh.360,000/=
2.	CRDB	Tsh.30,000/=	Tsh.360,000/=
3.	POSTAL	Tsh.30,000/=	Tsh.360,000/=
4.	TTCL	Tsh.30,000/=	Tsh.360,000/=
5.	TANESCO	Tsh.30,000/=	Tsh.360,000/=
6.	MAKAMPUNI MENGINE	Tsh.30,000/=	Tsh.360,000/=

Sheria Ndogo Za (Usafi wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea.)

JEDWALI LA PILI

ILANI YA KUONDOA KERO
(Chini ya kifungu cha 42)

Ilani hii imetolewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo za Afya na Usafi wa Mazingira za Halmashauri ya Mji Kondoa, 20....

SEHEMU ‘A’

Ndugu.....wa
Mtaa/Kijiji.....Kata
ya.....Uliofanyika
Unaarifiwa kwamba katika ukaguzi
Tarehe.....mwezi.....mwaka.....
Katika nyumba yako ya Biashara/kuishi/kutolea Huduma/kiwanja* iliyopo eneo la.....k
umekutwa machukizo/kero/uchafu* kama ifuatavyo;

- 1)
2)
3)

SEHEMU ‘B’

Kwa ilani hii unaamriwa kurekebisha/kuondoa/kusafisha* kwa;

1.
2.
3.

SEHEMU ‘C’

Unapewa muda wa siku saba (7) tangu siku ya kupokea ilani hii, unatakiwa kutekeleza yote yaliyoelezwa katika sehemu ‘B’ ya Ilani hii, kushindwa kwako kutekeleza ndani ya muda uliopewa Halmashauri italazimika kukuchukulia hatua kali za kisheria bila kulazimika kukupa taarifa nyingine.

Sheria Ndogo Za (Usafi wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea.)

IMETOLEWA NA;

IMEPOKELEWA NA;

Jina; Jina;

Saini; Saini;

Wadhifa..... Wadhifa;

Tarehe..... Tarehe;

*Futa lisilohusika

Sheria Ndogo Za (Usafi wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea.)

JEDWALI LA TATU
(Chini ya kifungu cha 41)

ILANI YA KUJENGA CHOO

Ilani hii imetolewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo za (Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Mji wa Kondoa, 20....

SEHEMU ‘A’

Ndugu.....wa	Mtaa/Kijiji
.....	Kata ya	
Unaarifiwa kwamba katika ukaguzi uliofanyika Tarehe.....	mwezi.....	
mwaka.....		
Katika nyumba yako ya Biashara/kuishi/kutolea Huduma*/ Namba.....		
iliyopo eneo la.....katika	
Kitongoji/Mtaa*.....	Kijiji cha	
Kata ya		
Imekuwa haina choo/ choo kimejaa/kimeharibika* hivyo unaamriwa kutekeleza		
mambo yafuatayo;		
(1)		
(2)		
(3)		
(4)		

SEHEMU ‘B’

Unapewa muda wa siku thelathini (30) tu tangu siku ya kupokea ilani hii kutekeleza maelekezo yote yaliyoelezwa katika sehemu ‘A’ ya Ilani hii,

SEHEMU ‘C’

Ukaguzi wa kuthibitisha utekelezaji wa maelekezo uliyopewa utafanyika tarehe Endapo utashindwa kutekeleza maelekezo ndani ya muda uliopewa Halmashauri itakuchukulia hatua kali za kisheria bila kukupa taarifa nyingine

AFISA MWIDHINIWA

Sheria Ndogo Za (Usafi wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea.)

IMETOLEWA NA;	IMEPOKELEWA NA;
Jina;	Jina;
Saini;	Saini;
Wadhifa;	Wadhifa;
Tarehe;	Tarehe;

*Futa lisilotakiwa

Sheria Ndogo Za (Usafi wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea.)

JEDWALI LA NNE

HATI YA KUFILISHA KOSA
(*Limetungwa Chini ya Kifungu cha 54*)

Mimi nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya..... ambaye ni mkurugenzi wa halmashauri ya mji kondoa kwamba mnamo tarehe ya mwezi..... Mwaka nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi za Usafi na Mazingira za Halmashauri ya Mji Kondoa za Mwaka 2018

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri niko tayari kulipa kiasi cha shilingi laki tatu (Tsh 300,000/=) kama faini ninaodaiwa.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA
NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe MweziMwaka

Jina:

Saini:

Mbele ya:

Cheo:

Saini:

Tarehe:

Sheria Ndogo Za (Usafi wa Mazingira) Za Halmashauri ya Mji Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea.)

Nembo ya Halmashauri ya Mji wa kondoa imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe 13/5/2017 mbele ya:-

KHALIFA KONDO
Mkurugenzi wa Mji
Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa

L.S

HAMZA MAFITA
Mwenyekiti
Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa

NAKUBALI,

DODOMA,
15 Agosti, 2018

SELEMANI S. JAFO (Mb.),
Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI